

DAWA YAKO: Hydrochlorothiazide (HCTZ) ____ mg

Kwanini ninapatiwa dawa hii? Una shinikizo la juu la damu. Shinikizo la juu la damu ni hatari iwapo halitotibiwa. Linaweza kusababisha viharusi na mishtuko ya moyo. Unaweza kupoteza maisha kwa kuwa na shinikizo la juu la damu ambalo halijatibiwa.

Meza kidonge 1 mara tu baada ya kuamka kila asubuhi. Hauhitaji kula kitu kabla ya kumeza kidonge hichi.

Nitajihisije nitakapokunywa dawa hii? Nyakati nyingine, huwa kuna athari za kimatibabu zinazotokana na kunywa dawa hii. Athari ya kimatibabu ni jambo lile unaloweza kujihisi ambalo si la kawaida. Baadhi ya athari za kimatibabu zinazotokana na kunywa HCTZ hutokea pindi mwili wako unapoanza kuizoea dawa hii na zinaweza kujumuisha kuharisha, kizunguzungu, kupoteza hamu ya kula, mchafuko wa tumbo, na maumivu ya kichwa.

Baadhi ya athari za kimatibabu huwa hazitokei mara nyingi, hata hivyo zinaweza kuwa kali sana. **Piga 911 au tembelea Chumba cha Dharura upesi kama utajihisi kupata: mabaka ya ngozi; kuvimba kwa uso, mdomo, ulimi ama koo; shida katika kupumua ama kukosa pumzi; maumivu ya macho/uhafifu katika kuona; ama, mkojo kidogo au kukosa mkojo.**

Nini kingine ninachopaswa kufahamu?

1. Unapaswa kunywa dawa hii kila siku hata pale utakapojihisi kuwa sawa.
2. Unapaswa kuijaza upya dawa hii kila mwezi.
3. Usinywe pombe. Kunywa maji mengi.
4. Kama utatembelea ofisi ya daktari tofauti, kliniki tofauti ya kitabibu ama chumba tofauti cha dharura, utapaswa kuwataarifu kwamba una shinikizo la juu la damu na kwamba unakunywa dawa ya Hydrochlorothiazide.
5. Kama utashika ujauzito, utabidi kuacha kunywa dawa hii upesi. Rudi Kiliniki ya Kitabibu ya Grace Village ili kuonana na daktari, ili tuweze kukupatia dawa nyingine ya shinikizo la juu la damu ya wewe kumeza.

“Maudhui haya ni ya kwa makusudi ya utoaji taarifa pekee na hayapaswi kuhesabiwa kuwa kama ushauri wa afya wa kitaalamu. Daima tafuta kupata ushauri kutoka kwa Tabibu wako ama mhudumu mwingine wa afya mwenye sifa, kuhusiana na maswali yoyote unayoweza kuwa nayo yanayohusu hali fulani ya kiafya au matibabu.”